


**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA  
UFUNDI STADI (NACTVET)**



**TAARIFA KWA UMMA  
MATOKEO YA UHAKIKI WA UDAHILI WA NYONGEZA NA  
MAREKEBISHO KATIKA PROGRAMU MBALIMBALI KWA MKUPUO WA  
SEPTEMBER, 2023/2024**

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linataarifu umma kuwa matokeo ya uhakiki wa sifa za walioomba kujiunga na programu mbalimbali kwa awamu ya nyongeza na marekebisho mkupuo wa septemba 2023/2024 yametoka rasmi leo tarehe 17 Oktoba, 2023.

Udahili kwa mwaka wa masomo 2023/2024 ulianza tarehe 21 Mei, 2023 hadi tarehe 16 Julai, 2023 kwa awamu ya kwanza na tarehe 17 Julai hadi 25, Septemba, 2023 kwa awamu ya pili. Waombaji wa programu za Astashahada na Stashahada walituma maombi ya kudahiliwa katika vyuo mbalimbali Tanzania Bara na visiwani. Vyuo vilipokea maombi ya waombaji kisha kufanya uchaguzi kulinganana sifa za programu zinazotolewa na vyuo hivyo.

Jumla ya wombaji **17,807** kutoka vyuo **287** walichaguliwa na vyuo, na kuwasilishwa NACTVET kwa ajili ya uhakiki kuanzia tarehe 03-10 Oktoba, 2023. Waombaji **16,310** sawa na (91.6%) ya waombaji wote (wanawake ni **12,884** (79%) na wanaume **3,426** (21%) wamekidhi vigezo vya kujiunga na programu walizochagua.

Aidha, jumla ya waombaji **1,497**, sawa na (8.4%) ya waombaji wote hawakuwa na vigezo vya kujiunga kwenye programu walizochagua, wanawake ni **726** (49.1 %) na wanaume ni **749** (50.9 %). Majina ya waombaji waliohakikiwa tayari yametumwa vyuoni.

Waombaji wote waliowasilishwa NACTVET kwa ajili ya uhakiki wametumiwa msimbo (code) kupitia namba za simu zilizowasilishwa na vyuo. Msimbo huo utatumika kuhakiki udahili wao na sifa kwenye programu walizochaguliwa kupitia tovuti ya NACTVET [www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz) kwa kubofya kitufe cha “**Verification results 2023**”

Waombaji waliochaguliwa na kuthibitishwa wanahimizwa kuwasili kwenye vyuo walivyochaguliwa na kuhakikisha kuwa wanasajiliwa ili kuanza masomo kama ilivyopangwa. Pia vyuo vina agizwa kuwasajili waombaji waliochaguliwa kwenye mfumo wa Baraza kwa mujibu wa kanununi na taratibu za udahili wa wanafunzi. Endapo chuo kitakiuka taratibu za udahili hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya chuo hicho.

**IMETOLEWA NA:  
OFISI YA KATIBU MTENDAJI  
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)  
17/10/2023**